

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



OFISI YA RAIS,  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA MANISPAA YA KINONDONI



## TAARIFA KWA UMMA

Mkurugenzi wa Manispaa ya Kinondoni anawatangazia wamiliki wote wa nyumba za kulala wageni (Guest House) kuwa, mnatakiwa kusajili upya nyumba zenu za kulala wageni kuanzia tarehe 01 hadi 15 Desemba 2023. Usajili utafanyika katika Ofisi zetu za Divisheni ya Biashara zilizopo jengo la Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, Magomeni. Usajili huu utahusisha pia nyumba za kulala wageni hata zenye chumba kimoja. Unatakiwa kufika katika Ofisi zetu za Divisheni ya Biashara ukiwa na kitabu cha kulala wageni (Register).

Baada ya tarehe 15/12/2023 msako mkali utafanyika na atakaye bainika kutosajili nyumba ya kulala wageni atachukuliwa hatua kali ya kisheria ikiwemo kulipishwa faini ya Shilingi Milioni Moja.

Tangazo hili limetolewa na Mkurugenzi wa Manispaa ya Kinondoni.

Leo Tarehe 22-11-2023